

# NIPASHHE

## Wagonjwa wanne wafanyiwa operesheni ya moyo India

Na Joseph Mwendapole

WAGONJWA wanne wa moyo kati ya 11 waliokwenda India kwa ajili ya matibabu mwanzoni mwa wiki iliyopita tayari wamefanyiwa upasuaji.

Kwa mujibu wa mratibu wa maradhi ya moyo katika klabu ya Lions ya Dar es Salaam (host), Dk. Rajni Kanabar, wagonjwa hao wamefanyiwa upasuaji wenye mafanikio makubwa.

Alisema wagonjwa wengine wataanza kufanyiwa upasuaji kuanzia wiki hii na wanatarajia kurejea nchini baada ya wiki tatu.

Wagonjwa hao waliondoka chini ya uratibu wa Lions Klabu na Hospitali ya Regency ya Dar es Salaam na Wizara ya Afya ya Zanzibar.

Dk. Kanabar alisema wagonjwa hao walipokelewa vyema na madaktari bingwa na wafanyakazi wa hospitali ya Fortis Escorts Heart Institute iliyoko mji wa New Delhi, India.

"Upasuaji wa wagonjwa wanne umefanyika bila kuwa na matatizo yoyote na wengine tunatarajia wiki hii

wataanza kufanyiwa upasuaji. Tunatarajia watapona vizuri na kurejea nyumbani ndani ya wiki tatu," alisema Dk. Kanabar.

Lion Dk. Rajni Kanabar alimshukuru balozi wa India Kocheril Bhagirath kwa kutoa visa bure kwa wagonjwa wote 11 na wasindikizaji wao na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Reginald Mengi, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya kuwaaga watoto hao katika hospitali ya Regency Dar es Salaam.

Wengine ni Said Bakhressa ambaye alisaidia fedha za upasuaji kwa watoto watatu na za kujikimu wakiwa kwenye matibabu na Wizara ya Afya ya Zanzibar kwa kutoa fedha za upasuaji kwa wagonjwa sita na tiketi na Shirika la Ndege la Emirates.

Dk. Kanabar alisema miongoni mwa watakaofanyiwa upasuaji yumo mtoto mdogo wa miezi tisa.

Alisema hospitali ya Escorts ni maarufu duniani kwa upasuaji wa moyo na imekuwa ikitoa punguzo la gharama kwa wagonjwa wanaotoka nchini Tanzania